

DUA ZA MIEZI
MITATU MITUKUFU
(Rajabu, Shaabani na Ramadhani)

Kimetarjumiwa na:
Sayyid Ahmed Aqyl

Kimehaririwa na:
Al-Haj Ramadhani S. K. Shemahimbo

YALIYOMO

Neno la mchapishaji	v
Utangulizi	6
Dua za Mwezi wa Rajabu	9
Dua ya Kwanza	9
Dua ya Pili.....	10
Dua ya Tatu	11
Dua ya Nne	12
Swala ya Mtume (s.a.w.w) katika	14
Mwezi wa Rajabu Munajaati wa Imam ‘Ali (a.s.) katika mwezi wa Shaabani –Munajaatish Shaabaniyyah	
Swala ya Mtume (s.a.w.w) katika mwezi	18
wa Shaabani	
Soma dua hizi baada ya kila swala ya faradhi	34
katika Mwezi wa Ramadhani	
Dua za Siku Maalumu za Mwezi Mtukufu	39
wa Ramadhani alizokuwa akizisoma Bwana Mtume (s.a.w.w.)	

© **Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**

Al-Itrah Foundation

ISBN No: 978-9987-427-05-5

Kimetarjumiwa na:

Sayyid Ahmed Aqyl

Kimehaririwa na:

Al-Hajj Ramadhani S. K. Shemahimbo

Toleo la kwanza: Machi 2013

Nakala:1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Al-Itrah Foundation

S.L.P. 19701, Dar Es Salaam. Tanzania

Simu: +255 22 2127555 / 2110640

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.ibn-tv.com

Katika mtandao: www.alitrah.info

Kwa kushirikiana na:

Idara ya Utamaduni

Ubalozi wa Jamhuri wa Kiislamu wa Iran

S.L..P 59595-00200

NAIROBI-KENYA

Simu: (+ 255) (2) 2214353 (+ 254) 713 836041

Barua pepe: iranlib@yahoo.com

Tovuti: http://www.nairobi.icro.ir

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni mkusanyiko wa dua mbalimbali ambazo zimetokana na Maasumina 14 (a.s) watokanao na nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w).

Bwana Mtume amesema: “Dua ni silaha ya muumini,” hivyo ni kinga kwake pia. Utaona kwamba dua ni kitu muhimu sana kwa waumini; na hiki ndicho kilichomsukuma ndugu yetu Sayyid Aqyl kuzikusanya dua hizi ambazo ni muhimu sana na kuzitarjumi kwa lugha ya Kiswahili, lakini pia bila kuiacha lugha yake ya asili ambayo ni ya Kiarabu kwenda sambamba na Kiswahili. Na hili kwa hakika litamrahisishia msomaji wa Kiswahili hali kadhalika na msomaji wa Kiarabu kuzielewa vizuri dua hizi.

Si mara ya kwanza kwa Sayyid Aqyl kuandika kitabu cha dua, kabla yake alitarjumi dua mashuhuri iitwayo, Dua Kumayl. Tunamshukuru sana kwa juhudi zake hizi za kuwahudumia waumini wenzake. Tunamuomba Allah ampe wasaa zaidi katika juhudi zake hizi, na ampe afya njema ili aweze kutekeleza wajibu huu.

Taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni chenye manufaa makubwa kwao.

Tunawashuku wale wote waliosaidia kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na huko Akhera pia. Amin!

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
Dar es Salaam

UTANGULIZI

Dua, yaani maombi si matamshi ya kutamkwa kwa ulimi tu, bali ni hali ya uhitaji wa moyoni inayodhihirishwa na ulimi. Panapokosekana mapatano baina ya yaliyo moyoni na matamshi ya ulimini, dua hiyo hukosa dhamira na kuwa mbali na rehema za Muumba, inabaki ni mfano wa kiumbe kisichokuwa na roho.

Dua kisheria ni njia bora ya mja kupata matakwa yake ya halali. Sheria za kimaumbile zinatuhimiza kutaka usaidizi kutoka kwa Muumba katika hali zote ziwazo. Hivyo nikusema kwamba hata katika zile hali ambazo mja mwenyewe anadhania anauezo nazo, asifikirie kwamba hana haja ya maombi.

Kwa upande mwingine, ni makosa mja kubaki kuomba na kuacha kutumia uwezo wa kawaida kufikia malengo na matilaba yake ya kila leo. Fikra hiyo ni ya kimakosa kwani huu ulimwengu umeumbwa juu ya kanuni zinazohukumu na kuendesha maisha ya mwanadamu. Mwenyezi Mungu pamoja na upeo wa uwezo Wake amekataa kuyapeleka mambo ila kwa kupitia sababu zake. Kinachoinuka hakiinuki ila kwa sababu zake, ingawa Mwenyezi Mungu anaweza kukiinua bila sababu hizo. Na kinachoanguka hakianguki ila kwa sababu zake, ingawa Mwenyezi Mungu anaweza kukiangusha bila ya sababu.

Dua ni ukumbi katika rehema za Mwenyezi Mungu na ina dauru kubwa katika maisha yetu. Umuhimu wa dua, mbali ya kuwa ni wa kiroho, pia ni ujenzi wa maadili mema. Kwa kutambua rehema ya Mwenyezi Mungu juu yetu, na sisi ki-maadili tunawahurumia wenzetu na kuwaombea mema kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Kupata majibu ya maombi yetu, inatakikana tuwe katika hali ya unyenyekevu na uwelekevu wa akili pale tunapomomba Mwenyezi Mungu. Mfano mzuri ni ule Mola aliomfunza Nabii Isa (a.s.) alipomwambia: “Ewe Isa unyenyekeze moyo wako Kwangu, unapojitenga pekeo na unitaje kwa wingi. Tambua kwamba furaha Yangu ni usononekee Kwangu na kuwa hai usiwe maiti (mwangalivu na sio mtepetevu), unifanye niisikie sauti yako ya huzuni.”

Dua hizi nilizozifasiri hapa, ni dua ambazo tumefunzwa na Ahlul-Bayt ambao Bwana Mtume (s.a.w.w.) alitutaka tushikamane nao. Rajabu, Shaabani na Ramadhani ni miezi ya fadhila nyingi. Bwana Mtume (s.a.w.w.) amepokewa akisema kwamba: “Rajabu ni mwezi mtukufu kuliko mwezi mwengine kwa heshima na fadhila. Katika mwezi huu Jihadi dhidi ya makafiri ni haramu. Rajabu ni mwezi wa Mwenyezi Mungu, Shaabani ni mwezi wangu na mwezi wa Ramadhani ni wa Umma wangu. Yeyote atakayefunga siku moja ya mwezi huu Mwenyezi Mungu atamuepusha mbali na adhabu, atakuwa radhi naye na atafungiwa mlango mmoja wa motoni.”

Imam Kadhvim (a.s.) amepokewa akisema kwamba: “Atakayefunga siku moja ya Rajabu, ataepushwa na moto wa Jahannamu kwa masafa ya mwaka mmoja. Na atakayefunga siku tatu basi wajibu wake ni kuingia Peponi.” Amepokewa tena kwamba amesema: “Rajabu ni jina la mto wa Peponi, weupe wake washinda weupe wa maziwa na utamu wake washinda asali, basi yeyote atakayefunga katika Rajabu atapata kunywa katika mto huo.”

Bwana Mtume (s.a.w.w.) amepokewa kwamba amesema: “Rajabu ni mwezi wakuomba maghufira, ombeni msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu s.w.t.”

Kuna amali nyingi na dua za kusomwa katika mwezi huu wa Rajabu, mimi hapa nimetabaruku kidogo tu, kwa rehema za Mwenyezi Mungu (s.w.t.). Atakaye zaidi aweza kuangalia katika vitabu vilivyokusanya dua na mafunzo ya Ahlul-Bayt kama vile *Mafaatihul Jinaani* na venginevyo. Mwisho kabisa natoa shukurani zangu kwa wale waliosaidia kukichapisha kitabu hiki, Mwenyezi Mungu awabariki.

Wabillahi tawfiq
Sayyid Ahmed Aqyl
(March 10, 2012)

DUA ZA MWEZI WA RAJABU

DUA YA KWANZA

Dua hii ya kwanza imependekezwa kusomwa baada ya kila swala ya faradhi katika mwezi huu wa Rajabu. Shaykh Abbas Qummi asema katika Mafaatihul Jinaani kwamba dua hii ilipatikana kutoka kwa Imam Ja'far as-Swadiq (a.s.).

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

يَا مَنْ أَرْجُوهُ لِكُلِّ خَيْرٍ وَأَمِنْ سَخَطِهِ عِنْدَ كُلِّ شَرٍّ، يَا مَنْ يُعْطِي الْكَثِيرَ بِلِقَلِيلٍ، يَا مَنْ يُعْطِي مَنْ سَأَلَهُ، يَا مَنْ يُعْطِي مَنْ لَمْ يَسْأَلْهُ وَمَنْ لَمْ يَعْرِفْهُ، تَحَنُّنًا مِنْهُ وَرَحْمَةً. أَعْطِنِي بِمَسْأَلَتِي إِيَّاكَ جَمِيعَ خَيْرِ الدُّنْيَا وَجَمِيعَ خَيْرِ الْآخِرَةِ، وَصَرِّفْ عَنِّي بِمَسْأَلَتِي إِيَّاكَ جَمِيعَ شَرِّ الدُّنْيَا وَشَرِّ الْآخِرَةِ، فَإِنَّهُ غَيْرُ مَنْقُوصٍ مَا أَعْطَيْتَ وَزِدْنِي مِنْ فَضْلِكَ يَا كَرِيمُ.

“Ewe ninayemtumainia kwa kila la kheri, na kusalimika na hasira Zake katika kila shari. Ewe Anayetoa kingi kwa kichache. Ewe Anayempa amuombaye, Ewe ambbaye humpatia asiyemuomba na asiyemtambua, yote ni kutokana na Yake

mapenzi na huruma. Niombalo Kwako Wewe tu ni unipe Kheri yote ya dunia na kheri yote ya akhera, na niombalo Kwako Wewe tu ni uniepshie shari yote ya dunia na akhera. Kwa amri na shani Yako, hakina upungufu Utoacho na nizidishie fadhila Zako, Ewe Mkarimu.”

Hapa Imam Ja'far (a.s.) alishika ndevu zake kwa mkono wa kushoto na akatingisha kidole cha shahada cha mkono wa kulia na kuendelea kusema maneno haya:

يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ يَا ذَا النِّعْمَاءِ وَالْجُودِ يَا ذَا الْمَنِّ وَالطُّوْلِ حَرَمٌ
شَيْبَتِي عَلَى النَّارِ

“Ewe Mwenye utukufu na ukarimu, Ewe Mwenye neema na upaji, Ewe Mwenye fadhila na muendeleza wema, uharamishe uzee wangu juu la moto.”

DUA YA PILI

Dua hii ni ya kusomwa kila siku hii ilikuwa ikisomwa na Imam Zaynul Abidiin (a.s.)

يَا مَنْ يَمْلِكُ حَوَائِجَ السَّائِلِينَ وَيَعْلَمُ ضَمِيرَ الصَّامِتِينَ، لِكُلِّ
مَسْأَلَةٍ مِنْكَ سَمْعٌ حَاضِرٌ وَجَوَابٌ عَتِيدٌ، اللَّهُمَّ وَمَوَاعِينُكَ
الصَّادِقَةُ، وَأَيَادِيكَ الْفَاضِلَةُ، وَرَحْمَتُكَ الْوَاسِعَةُ، فَاسْأَلُكَ أَنْ

تُصَلِّيَ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَأَنْ تَقْضِيَ حَوَائِجِي لِلدُّنْيَا
وَالْآخِرَةِ، إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Ewe Unayezimiliki haja za waombaji na Unayezijua dhambi za wanyamavu, Kila ombi Kwako hupata usikizi tayari na ufumbuzi madhubuti. Ewe Mwenyezi Mungu, nakuomba kwa haki ya ahadi Zako za kweli, na ubora wa vipawa Vyako na ue-nevu wa rehema Zako. Mrehemu Muhammad na aali Muhammad, Unikidhie haja zangu za dunia na Akhera, kwani Wewe ni Muweza juu ya kila kitu.”

DUA YA TATU

Dua hii Imam Ja'far as-Swadiq (a.s.) alikuwa akiisoma kila siku

خَابَ الْوَافِدُونَ عَلَى غَيْرِكَ، وَخَسِرَ الْمُتَعَرِّضُونَ إِلَّا لَكَ،
وَضَاعَ الْمُلْمُونَ إِلَّا بِكَ، وَأَجْدَبَ الْمُتَتَجِعُونَ إِلَّا مَنْ انْتَجَعَ
فَضْلَكَ، بِأَبْكَ مَفْتُوحٌ لِلرَّاعِيَيْنِ وَخَيْرُكَ مَبْدُولٌ لِلطَّالِبِينَ،
وَفَضْلُكَ مُبَاحٌ لِلسَّائِلِينَ وَنَيْلُكَ مُتَاحٌ لِلْأَمْلِينَ، وَرِزْقُكَ
مَبْسُوطٌ لِمَنْ عَصَاكَ وَحِلْمُكَ مُعْتَرِضٌ لِمَنْ نَوَاكَ، عَادَتُكَ
الإِحْسَانُ إِلَى الْمُسِيئِينَ، وَسَبِيلُكَ الإِبْقَاءُ عَلَى الْمُعْتَدِينَ

اللَّهُمَّ فَهْدِنِي هُدَى الْمُهْتَدِينَ، وَرَزُقْنِي إِجْتِهَادَ الْمُجْتَهِدِينَ،
وَلَا تَجْعَلْنِي مِنَ الْعَافِلِينَ الْمُبْعَدِينَ، وَغْفِرْ لِي يَوْمَ الدِّينِ

“Wamedata waliomfungia safari asiyekuwa Wewe, na wana hasara wadadisi ila kwa sababu Yako, wamepotea wanaojitolea ila kwa ajili Yako, na wamekaukiwa wenye kuji-faidisha ila aliyefaidika kwa fadhila Zako. Mlango Wako uko wazi kwa wenye raghba, na kheri Yako hutolewa kwa wingi kwa wenye kuitaka. Fadhila Zako huwafikia wanaoziom-ba, tunu Zako humfikia kila anayezitazamia na riziki Yako huandaliwa wenye kukuasi pia. Upole Wako umewakinga hata wanaokufanyia uadui, ni ada Yako kuwafanyia wema waovu na mwenendo Wako ni kuwapa muhula wanaopituka mipaka. Basi Eee Mwenyezi Mungu, niongoe uongofu wa walioongoka, Uniruzuku jitihada ya wenye juhudi, na Usinijaalie kuwa miongoni mwa walioghafilika waliotengwa, na Unighufirie Siku ya malipo.”

DUA YA NNE

Amesema Shaykh Mis’bah kwamba imepokewa kutoka kwa Al-Ma’ali b. Khunais kwamba Imam Ja’far as-Swadiq (a.s.) amesema soma dua hii. Na katika al-Iqbaal amedokeza kuwa dua hii imebeba maombi mengi, na yafaa isomwe kila wakati.

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ صَبْرَ الشَّاكِرِينَ لَكَ، وَعَمَلَ الْخَائِفِينَ مِنْكَ،

وَيَقِينِ الْعَابِدِينَ لَكَ. اللَّهُمَّ أَنْتَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ، وَأَنَا عَبْدُكَ
 الْبَائِسُ الْفَقِيرُ، أَنْتَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ، وَأَنَا الْعَبْدُ الذَّلِيلُ. اللَّهُمَّ
 صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ، وَمَنْ بَعْنَاكَ عَلَى فَقْرِي، وَبِحَلْمِكَ
 عَلَى جَهْلِي، وَبِقُوَّتِكَ عَلَى ضَعْفِي، يَا قَوِي يَا عَزِيزُ. اللَّهُمَّ
 صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ الْأَوْصِيَاءِ الْمَرْضِيِّينَ، وَكَفِنِي مَا أَهَمَّنِي
 مِنْ أَمْرِ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, mimi nakuomba subira ya wenye shukurani Kwako na amali za wenye kuhofia Kwako, na yakini ya wenye kukuabudu. Ewe Mwenyezi Mungu! Wewe ndiwe Mtukufu Adhimu na mimi ni mja Wako masikini hoi, Wewe ndiwe Mkwasi Msifiwa na mimi ni mja mnyonge. Ewe Mwenyezi Mungu mrehemu Muhammad na aalize, Unifadhili kwa ukwasi Wako juu ya umasikini wangu na kwa upole Wako juu ya ujinga wangu, na kwa nguvu Zako juu ya udhai-fu wangu, Ewe Mwenye nguvu Ewe Mshindi. Ewe Mwenyezi Mungu mrehemu Muhammad na aalize mawasii walioridhi-wa, Unikifie mambo yanayonikera ya dunia na ya Akhera, Ewe Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.”

SWALA YA MTUME (S.A.W.W.) KATIKA MWEZI WA RAJABU

Hii ni swala maalumu kwa ajili ya kumtakia Bwana Mtume (s.a.w.w.) rehema mwezi huu:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

اللَّهُمَّ يَا ذَا الْمَنِّ السَّابِغَةِ، وَالْأَلَاءِ الْوَارِعَةِ، وَالرَّحْمَةِ الْوَاسِعَةِ،
وَالْقُدْرَةِ الْجَامِعَةِ، وَالنِّعْمَةِ الْجَسِيمَةِ، وَالْمَوَاهِبِ الْعَظِيمَةِ،
وَالْأَيَادِي الْجَمِيلَةَ، وَالْعَطَايَا الْجَزِيلَةَ.

“Ewe Mwenyezi Mungu, Ewe Mwingi wa fadhila kubwa kubwa na mipangilio ya kheri, na rehema zilizosambaa na uwezo wote, na neema za maana na tunu za fakhari, na vipawa vizuri na upaji wa kutosheleza.

يَا مَنْ لَا يُنْعَتُ بِتَمَثِيلٍ وَلَا يُمَثَّلُ بِنَظِيرٍ وَلَا يُغْلَبُ بِظَهِيرٍ، يَا مَنْ
خَلَقَ فَرَزَقَ، وَالْهَمَّ فَأَنْطَقَ، وَابْتَدَعَ فَشَرَعَ، وَعَلَى فَرْتَفَعَ، وَقَدَّرَ
فَأَحْسَنَ، وَصَوَّرَ فَأَتَقَنَ، وَاحْتَجَّ فَأَبْلَغَ، وَأَنْعَمَ فَأَسْبَغَ، وَأَعْطَى
فَأَجْزَلَ، وَمَنَّحَ فَأَفْضَلَ.

“Ewe Asiyesifiwa kwa mifano na hafananishwi na umbo, wala hashindwi kwa kutokewa. Ewe Aliyeumba na kuruzuku, Aliyefahamisha na kunenesha, Aliyezua na kuongoa, Aliyetukuza na kuinua, Aliyekadiria na kupanga vizuri, Aliyetengeneza umbile na kulimaizisha uyakini, Aliyetoa hoja fika na upambanuzi, Akaneemesha na kuzieneza, Akatoa na Akakithirisha kusambaza, Akagawanyiza na kufadhilisha.”

يَا مَنْ سَمَا فِي الْعِزِّ فَفَاتَ نَوَاطِرَ الْأَبْصَارِ، وَدَنَا فِي اللَّطْفِ
فَجَازَ هَوَاجِسَ الْأَفْكَارِ. يَا مَنْ تَوَحَّدَ بِالْمُلْكِ فَلَا نَدَّ لَهُ فِي
مَلَكُوتِ سُلْطَانِهِ، وَتَفَرَّدَ بِالْإِلَاءِ وَالْكَبْرِيَاءِ فَلَا ضِدَّ لَهُ فِي
جَبْرُوتِ شَأْنِهِ. يَا مَنْ حَارَتْ فِي كِبْرِيَاءِ هَيْبَتِهِ دَقَائِقُ لَطَائِفِ
الْأَوْهَامِ، وَانْحَسَرَتْ دُونَ إِدْرَاكِ عَظَمَتِهِ حَطَائِفُ أَبْصَارِ الْأَنَامِ.

“Ewe Ambaye ni kilele cha utukufu, Aliyeyabandua maanga ya maono, na kwa mapenzi Akaafiki kuruhusu uchambuzi wa mawazo. Ewe Aliyepwekeka kwa ufalme, Asiye na mshirika katika utawala Wake, Asiye kifani kwa neema na Ukuu, na hana mpinzani kwa utenza wa jambo Lake. Ewe Aliyezipa uhuru dhana ndogondogo kwa ukuu wa haiba Yake, umeshindwa ukaguzi wa macho ya waja kuuona utukufu Wake.”

يَا مَنْ عَنَتِ الْوُجُوهُ لِهَيْبَتِهِ، وَخَضَعَتِ الرَّقَابُ لِعَظَمَتِهِ،
 وَوَجَلَتِ الْقُلُوبُ مِنْ خِيفَتِهِ. أَسْأَلُكَ بِهَذِهِ الْمِدْحَةِ الَّتِي لَا تَنْبَغِي
 إِلَّا لَكَ، وَبِمَا وَآيَتَ بِهِ عَلَي نَفْسِكَ لِذَاعِيكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ،
 وَبِمَا ضَمِنْتَ الْإِجَابَةَ فِيهِ عَلَي نَفْسِكَ لِلدَّاعِينَ. يَا أَسْمَعَ
 السَّمَاعِينَ وَأَبْصَرَ النَّاطِرِينَ وَأَسْرَعَ الْحَاسِبِينَ، يَا ذَا الْقُوَّةِ
 الْمَتِينِ، صَلِّ عَلَي مُحَمَّدٍ خَاتَمِ النَّبِيِّينَ وَعَلَي أَهْلِ بَيْتِهِ، وَأَقْسِمُ
 لِي فِي يَوْمِي هَذَا خَيْرَ مَا قَسَمْتَ وَاحْتَمَّ لِي فِي قَضَائِكَ خَيْرَ
 مَا حَتَمْتَ، وَاحْتَمَّ لِي بِالسَّعَادَةِ فِي مَنْ خَتَمْتَ، وَأَحِينِي مَا
 أَحْيَيْتَنِي مَوْفُورًا، وَأَمْتِنِي مَسْرُورًا وَمَغْفُورًا، وَتَوَلَّ أَنْتَ نَحَاتِي
 مِنْ مُسَاءَلَةِ الْبَرْزَخِ، وَادْرَأْ عَنِّي مُنْكَرًا وَنَكِيرًا، وَارْ عَيْنِي مَبْشَرًا
 وَبَشِيرًا، وَاجْعَلْ لِي إِلَي رِضْوَانِكَ وَجَنَانِكَ مَصِيرًا وَعَيْشًا قَرِيرًا
 وَمُلْكًا كَبِيرًا. وَصَلِّ اللَّهُ عَلَي مُحَمَّدٍ وَآلِهِ كَثِيرًا.

“Ewe Ambaye nyuso zimemkongowea kwa haiba Yake, shingo zimemuinamia kwa utukufu Wake, na nyoyo hushikwa ni kiwewe kwa utisho Wake. Nakuomba kwa sifa hizi ambazo hazielekei ila Kwako na kwa ahadi Uliyojiwekea juu ya nafsi Yako, kwa akuombae kati ya waumini na kwa uliyoyadhami-

ni juu ya nafsi Yako kuwaitika wanaokulingania. Ewe Mwingi wa kusikia, Mwingi wa kuona na Mwepesi wa kuhisabu, Ewe Mwenye nguvu madhubuti.” Mrehemu Muhammad, mwisho wa mitume na watu wa nyumba yake. Nigawie katika siku yangu hii kheri unayoigawa, na nifaradhie kwa uamuzi Wako bora ya faradhi, nihitimishe kwa furaha ya unaowahitimisha, na nihuishe maisha ya maridhawa, unifishe nikiwa ni mwenye furaha mwenye kughufiriwa. Unitawalie Wewe uokozi wangu nitakapoulizwa hapo barzakhi, univushe mbali na Munkari na Nakiri na Uyaonyeshe macho yangu mawili Bashiri na Bishara. Unijaalie nirejee katika radhi Zako na Pepo Yako na maisha ya utulivu na uwezo mkubwa. Rehema nyingi za Mwenyezi Mungu zimteremkie Muhammad na alize.

MUNAJAATI WA IMAM ALI (A.S.) KATIKA MWEZI WA SHAABA- NI MAARUFU - MUNAJAATISH- SHAABANIYYA

Imepokewa kwamba Amiril Mu'miniin Imam Ali b. Abi Twalib (a.s.) pamoja na Maimamu wa kizazi chake (a.s.) walikuwa wakiisoma dua hii katika mwezi wa Shaabani.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ وَأَسْمَعْ دُعَائِي إِذَا دَعَوْتُكَ
وَسَمِعْ نِدَائِي إِذَا نَادَيْتُكَ وَأَقْبِلْ عَلَيَّ إِذَا نَاجَيْتُكَ فَقَدْ هَرَبْتُ
إِلَيْكَ وَوَقَفْتُ بَيْنَ يَدَيْكَ مِسْكِينًا مُتَضَرِّعًا إِلَيْكَ رَاجِيًا لِمَا
لَدَيْكَ ثَوَابِي

“Ewe Mwenyezi Mungu, mrehemu Muhammad na aali zake Muhammad, Unisikize ombi langu nikuombapo, niitikie wito wangu nikuitapo na geukia kwangu ninapokunong'oneza. Kwani nimekimbilia Kwako na nimesimama mbele Zako, nikiwa Kwako ni muhitaji mnyenyekevu, nikitaraji kutoka Kwako malipo mema.”

وَتَعَلَّمْ مَا فِي نَفْسِي وَتَخْبِرْ حَاجَتِي وَتَعْرِفْ ضَمِيرِي وَلَا يَخْفَى
عَلَيْكَ أَمْرٌ مُنْقَلَبِي وَمَثْوَايَ وَمَا أُرِيدُ أَنْ أُبْدِيَءَ بِهِ مِنْ مَنْطِقِي
وَأَتَفَوَّهُ مَنْ طَلَبْتِي وَأَرْجُوهُ لِعَاقِبَتِي

“Walijua la moyoni mwangu na waielewa haja yangu na waitambua nia yangu, wala Kwako sio lakufitika langu jambo la marejeo yangu na makao yangu; na ambayo ningetaka niyadhihirishe kwa usemi wangu na kuelezea ya matokeo yangu ninayoyatarajia.

وَقَدْ جَرَتْ مَقْدِيرُكَ عَلَيَّ يَا سَيِّدِي فِي مَا يَكُونُ مِنِّي إِلَى آخِرِ
عُمْرِي مِنْ سَرِيرَتِي وَعَلَانِيَتِي وَبِيَدِكَ لَا بِيَدِ غَيْرِكَ زِيَادَتِي
وَنَقْصِي وَنَفْعِي وَضُرِّي

“Na yamekwisha pita uliyonikadiria Ee Bwana wangu, yenye kunitukia mpaka mwisho wa umri wangu, yawe ni ya siri na ya dhahiri. Na ni kwa mkono Wako si kwa mkono wa mwingine kupata kwangu la ziada au upungufu, la manufaa yangu au la madhara yangu.

إِلَهِي إِنَّ حَرَمَتِي فَمَنْ ذَا الَّذِي يَرْزُقُنِي وَإِنْ خَذَلْتَنِي فَمَنْ ذَا

الَّذِي يَنْصُرُنِي؟ إِلَهِي أَعُوذُ بِكَ مِنْ غَضَبِكَ وَحُلُولِ سَخَطِكَ
 إِلَهِي إِنَّكَ تُغَيِّرُ مُسْتَأْهِلٍ لِرَحْمَتِكَ فَأَنْتَ أَهْلٌ أَنْ تَجُودَ عَلَيَّ
 بِفَضْلِ سَعَتِكَ

“Mola wangu iwapo utaninyima ni nani wa kuniruzuku; na iwapo utanitelekeza ni nani wakuninusuru? Mola wangu najilinda Kwako kutokana na ghadhabu Zako na kustahili kwangu kuteremkiwa na hasira Zako. Mola wangu iwapo si stahiki kupata rehema Zako, basi Wewe ni laiki Yako kunipa kwa fadhila za ukwasi Wako.”

إِلَهِي كَأَنِّي بِنَفْسِي وَأَقْفَةٌ بَيْنَ يَدَيْكَ وَقَدْ أَظْلَمَ حُسْنُ تَوَكُّلِي
 عَلَيْكَ فَقُلْتُ مَا أَنْتَ أَهْلُهُ وَتَعَمَّدْتَنِي بِعَفْوِكَ إِلَهِي إِنْ عَفَوْتَ
 فَمَنْ أَوْلَى مِنْكَ بِذَلِكَ وَإِنْ كَانَ قَدْ دَنَا أَجَلِي وَلَمْ يَدْنِنِي مِنْكَ
 عَمَلِي فَقَدْ جَعَلْتُ الْإِقْرَارَ بِالذَّمِّ إِلَيْكَ وَسَيِّئِي

“Mola wangu ni kana kwamba pekee nafsi yangu imesimama mbele Zako, imesitiriwa kwa wema wa utegemevu wangu Kwako, nikatamka ya laiki Yako, na ukanitanda kwa msamaha Wako. Mola wangu ukinisamehe, hebu ni yupi aula wa hilo kuliko Wewe? Na iwapo ajali yangu imekaribia na amali yangu haikunikurubisha Kwako, basi nimejaalia kuungama kwangu dhambi zangu ni wasila wangu Kwako.

إِلَهِي قَدْ جَرَتْ عَلَيَّ نَفْسِي فِي النَّظَرِ لَهَا فَلَهَا الْوَيْلُ إِنْ لَمْ
تَغْفِرْ لَهَا إِلَهِي إِنْ لَمْ يَزَلْ بَرُكَ عَلَيَّ أَيَّامَ حَيَاتِي فَلَا تَقْطَعْ بَرُكَ
عَنِّي فِي مَمَاتِي إِلَهِي كَيْفَ آيَسُ مِنْ حُسْنِ نَظَرِكَ لِي بَعْدَ
مَمَاتِي وَأَنْتَ لَمْ تُؤَلِّني إِلَّا الْجَمِيلَ فِي حَيَاتِي

“Mola wangu nimeikosea nafsi yangu kwa kuielekea, basi welewe! iwapo hutaisamehe. Mola wangu, wema Wako muda wa uhai wangu haukukoma, basi usinikatizie wema Wako katika kufa kwangu. Mola wangu vipi nitamauke juu ya ulinzi Wako mwema baada ya kifo changu! Na Wewe hukunipa ila mazuri katika uhai wangu.”

إِلَهِي تَوَلَّ مِنْ أَمْرِي مَا أَنْتَ أَهْلُهُ وَعَدَّ بِفَضْلِكَ عَلَيَّ مُذْنِبٍ قَدْ
غَمَرَهُ جَهْلُهُ إِلَهِي قَدْ سَتَرْتَ عَلَيَّ ذُنُوبًا فِي الدُّنْيَا وَأَنَا أَحْوَجُ
إِلَى سِتْرِهَا عَلَيَّ مِنْكَ فِي الْآخِرَةِ إِلَهِي قَدْ أَحْسَنْتَ إِلَيَّ إِذْ لَمْ
تُظْهِرْهَا لِأَحَدٍ مِنْ عِبَادِكَ الصَّالِحِينَ فَلَا تَفْضَحْنِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ
عَلَى رُؤُوسِ الْأَشْهَادِ

“Mola Wangu yatawali mambo yangu kama ilivyo laiki Yako, na kwa fadhila Zako muhisabu mtenda dhambi, aliyefunikizwa niujinga wake. Mola Wangu duniani ulinisitiria

dhambi zangu, na mimi nimuhitaji zaidi wakusitiriwa hayo Kwako katika Akhera. Mola Wangu tayari umenitendea vizuri kwa kutoyadhahirisha mbele za awaye kati ya waja Wako wema, basi usinifedhehi Siku ya Kiyama mbele za wenye kunishuhudia.”

إِلَهِي جُودُكَ بَسَطَ أَمَلِي وَعَفْوُكَ أَفْضَلُ مِنْ عَمَلِي إِلَهِي فَسُرَّنِي
بِلِقَائِكَ يَوْمَ تَقْضِي بِهِ بَيْنَ عِبَادِكَ

“Mola Wangu upaji Wako umenipanulia tumaini langu, na msamaha Wako ni bora kuliko amali yangu. Mola Wangu basi nifurahisha nifikapo Kwako Siku ya kuhukumu baina ya waja Zako.”

إِلَهِي إِعْتِدَارِ إِلَيْكَ إِعْتِدَارُ مَنْ لَمْ يَسْتَعِنْ عَنِ قَبُولِ عُذْرِهِ فَقَبْلِ
عُذْرِي يَا أَكْرَمَ مَنْ اِعْتَدَرَ إِلَيْهِ الْمُسِيئُونَ إِلَهِي لَا تَرُدِّحَاجَتِي
وَلَا تُخَيِّبْ طَمَعِي وَلَا تَقْطَعْ مِنْكَ رَجَائِي وَأَمَلِي

“Mola Wangu udhuru wangu Kwako ni udhuru wa asiye kuwa na udhuru wa kukubalika, basi hali iwavyo nikubalia udhuru wangu Ewe Mwingi wa ukarimu kwa watenda mao-vu wanaomtaradhia. Mola wangu usinikatalie haja yangu na usinikatishe tamaa yangu, na usiikate tamaa yangu na tumaini langu Kwako.”

إِلَهِي لَوْ أَرَدْتَ هَوَانِي لَمْ تَهْدِنِي وَلَوْ أَرَدْتَ فَضِيحَتِي لَمْ
تُعَافِنِي إِلَهِي مَا أَظْنُكَ تَرُدَّنِي فِي حَاجَةٍ قَدْ أَفْنَيْتُ عُمْرِي فِي
طَلِبِهَا مِنْكَ

“Mola Wangu ungetaka kunitweza usingeniongoza, na ungetaka kunifedhehi usingeniafu; Mola Wangu! hata sikudhanii, kuwa utanikatalia jambo ambalo nimelimalizia umri wangu kulitaka kutoka Kwako.”

إِلَهِي فَلَكَ الْحَمْدُ أَبَدًا دَائِمًا سَرْمَدًا يَزِيدُ وَلَا يَبِيدُ كَمَا تُحِبُّ
وَتَرْضَى إِلَهِي إِنْ أَخَذْتَنِي بِجُرْمِي أَخَذْتُكَ بِعَفْوِكَ وَإِنْ أَخَذْتَنِي
بِذُنُوبِي أَخَذْتُكَ بِمَغْفِرَتِكَ وَإِنْ أَدْخَلْتَنِي النَّارَ أَعْلَمْتُ أَهْلَهَا أَنِّي
أُحِبُّكَ

“Mola Wangu sifa njema zote ni Zako milele, daima, mfululizo zenye kuzidi zisokoma kama upendavyo na kuridhika. Mola Wangu ukinipatiliza kwa makosa yangu nitakushikilia kwa usamehevu Wako, na ukinipatiliza kwa dhambi zangu nitakushikilia kwa maghufira Yako, na unitiapo motoni, kwa ukweli nitawatangazia watuwe humo, mimi nakupenda.”

إِلَهِي إِنْ كَانَ صَعْرٌ فِي جَنْبِ طَاعَتِكَ عَمَلِي فَقَدْ كَبُرَ فِي جَنْبِ
رَجَائِكَ أَمَلِي إِلَهِي كَيْفَ أَتَقَلَّبُ مِنْ عِنْدِكَ بِالْخِيَّةِ مَحْرُومًا
وَقَدْ كَانَ حُسْنُ ظَنِّي بِجُودِكَ أَنْ تَقْلِبَنِي بِنَجَاةٍ مَرْحُومًا

“Mola Wangu ikiwa kuwiana na utwi’ifu wangu Kwako, ulimchache wa vitendo, basi matumaini yangu kulingana na ninayoyatarajia Kwako yalimakubwa. Mola Wangu vipi niondoke nikiwa nimetengwa na kufukuzwa kutoka Kwako, hali nakutazamia kwa mazuri Yako utaninusuru niwe ni mwenye kurehemewa.

إِلَهِي وَقَدْ أَفْنَيْتُ عُمْرِي فِي شِرَّةِ السَّهْوِ عَنكَ وَأَبْلَيْتُ شَبَابِي
فِي سَكْرَةِ التَّبَاعُدِ مِنْكَ إِلَهِي فَلَمْ أَسْتَيْقِظْ أَيَّامَ اغْتِرَارِي بِكَ
وَرُكُونِي إِلَى سَبِيلِ سَخَطِكَ

“Mola Wangu umri wangu nimeutumia kwa dhambi ya kukusahau, nikaudhuru ujana wangu kwa shibe nikajitenga Nawe. Mola Wangu sikuzindukia Kwako majira ya kughurika kwangu, nikaelekea kupata ghadhabu Zako.

إِلَهِي وَأَنَا عَبْدُكَ وَأَبْنُ عَبْدَيْكَ قَائِمٌ بَيْنَ يَدَيْكَ مُتَوَسِّلٌ بِكَرَمِكَ
إِلَيْكَ إِلَهِي أَنَا عَبْدٌ أَتَنَصَّلُ إِلَيْكَ مِمَّا كُنْتُ أَوَاجِهُكَ بِهِ مِنْ قَلَّةٍ

اسْتِحْيَائِيْمِنْ نَظْرِكَ وَأَطْلُبُ الْعَفْوَ مِنْكَ إِذِ الْعَفْوَ نَعْتُ لِكْرَمِكَ

“Mola Wangu mimi ni mja Wako mtoto wa waja Zako wawili, nakuomba na kukuelekea kwa ukarimu Wako. Mola Wangu mja mimi nataka kujitoa makosani Kwako, kwa ambayo nilikuwajihhi nayo mbele ya macho Yako kwa utovu wangu wa haya, na nakutaka msamaha kwani usamehevu ni moja ya sifa za ukarimu Wako.

إِلَهِي لَمْ يَكُنْ لِي حَوْلٌ فَأَنْتَقِلُ بِهِ عَنْ مَعْصِيَتِكَ إِلَّا فِي وَقْتٍ
أَيَقْطُنِي لِمَحَبَّتِكَ وَكَمَا أَرِدْتُ أَنْ أَكُونَ كُنْتُ فَشَكَرْتُكَ
بِإِذْخَالِي فِي كْرَمِكَ وَلِتَطْهِيْرَ قَلْبِي مِنْ أَوْسَاحِ الْعَفْلةِ عَنكَ

“Mola Wangu sikuwa na mbinu ya kujiepusha nisikuasi, ila pale unaponizindua kwa mahaba Yako, na kama ulivyo-taka niwe nimekuwa, basi nakushukuru kwa kunitia katika karama Zako, na kuutakasa moyo wangu kuuondolea uchafu wa kughafilika Nawe.

إِلَهِي أَنْظِرْ إِلَيَّ نَظْرَ مَنْ نَادَيْتَهُ فَأَجَابَكَ وَاسْتَعْمَلْتَهُ لِمَعْوَتِكَ
فَأَطَاعَكَ يَا قَرِيْبًا لَا يُبْعَدُ عَنِ الْمُعْتَرِّ بِهِ وَيَا جَوَادًا لَا يَبْنَحُلُ عَنِ
مَنْ رَجَا ثَوَابَهُ إِلَهِي هَبْنِي قَلْبًا يُدْنِيهِ مِنْكَ شَوْفُهُ وَلِسَانًا يُرْفَعُ
إِلَيْكَ صِدْقُهُ وَنَظْرًا يُقَرِّبُهُ مِنْكَ حَقُّهُ

“Mola Wangu niangalia kwa jicho la uliyemwita akakuitika, ukamtumisha na kwa muawana Wako akakutwii. Ewe wa karibu Usiyembali kwa anayemtapia, Ewe Mpaji Usiyemkatalia anayekutarajia kwa malipo mema. Mola Wangu nipe moyo wa shauku wa kuuvutia Kwako, na ulimi wa ukweli ukutukuze, na mtazamo hakika yake ni kunikuribisha Kwako.

إِلَهِي إِنْ مَنْ تَعَرَّفَ بِكَ غَيْرُ مَجْهُولٍ وَمَنْ لَادَ بِكَ غَيْرُ مَبْدُولٍ
وَمَنْ أَقْبَلَتْ عَلَيْهِ غَيْرُ مَمْلُولٍ إِلَهِي إِنْ مَنْ انْتَهَجَ بِكَ لِمُسْتَنِيرٍ
وَإِنْ مَنْ اعْتَظَمَ بِكَ لِمُسْتَجِيرٍ وَقَدْ لُدْتُ بِكَ يَا إِلَهِي فَلَا تُخَيِّبْ
ظَنِّي مِنْ رَحْمَتِكَ وَلَا تَحْجُبْنِي عَنْ رَأْفَتِكَ

“Mola Wangu hakika anayejitambulisha Kwako si waku-tojulikana, na anaefiki Yako si wakukaukiwa, na Unaemu-elekea si wa kusumbuka. Mola Wangu hakika anaekutakasia moyo ni mwenye kuwa na nuru, na anayekutukuza amepata ukombozi. Mola Wangu, Kwako tayari nimeuelekeza moyo wangu, basi usiniondolee rehema Zako ninazozizingatia na usinikatalie uraufu Wako.

إِلَهِي أَقْمِنِي فِي أَهْلِ وَوَلَايَتِكَ مَقَامَ مَنْ رَجَا الزِّيَادَةَ مِنْ مَحَبَّتِكَ
إِلَهِي وَالْهَمْنِي وَلَهَا بِذِكْرِكَ إِلَى ذِكْرِكَ وَاجْعَلْ هَمِّي إِلَى رَوْحِ
نَجَاحِي أَسْمَائِكَ وَمَحَلِّ قُدْسِكَ إِلَهِي بِكَ عَلَيْكَ إِلَّا الْحَقَّتْنِي

بِمَحَلِّ أَهْلِ طَاعَتِكَ وَالْمَثْوَايِ الصَّالِحِ مِنْ مَرْضَاتِكَ فَإِنِّي لَا
أَقْدِرُ لِنَفْسِي دَفْعًا وَلَا أَمْلِكُ لَهَا نَفْعًا

“Mola Wangu niweke pamoja na mawalii Wako, pamoja na anayetazamia kuzidishiwa mahaba Yako. Mola Wangu nipe ilhamu kwa ukumbusho Wako kwa shauku nikudhukuru, uifanye hamu yangu ni kufurahia majina Yako matukufu na kupata pahala pa utakatifu Wako. Mola Wangu nikutakalo silengine ila kwa usaidizi Wako uniweke pamoja na wanaokutwii na makazi mema ya maridhia Yako, kwani mimi siwezi kuulinda nafsi yangu wala sina wasaa wa kuifalia jambo.

إِلَهِي أَنَا عَبْدُكَ الضَّعِيفُ الْمَذْنِبُ وَمَمْلُوكُكَ الْمُنِيبُ فَلَا
تَجْعَلْنِي مِمَّنْ صَرَفَتْ مِنْهُ وَجْهَكَ وَحَجَبَهُ سَهْوُهُ عَنْ عَفْوِكَ
إِلَهِي هَبْ لِي كَمَالَ الْإِنْقِطَاعِ إِلَيْكَ وَأَنْزِرْ أَبْصَارَ قُلُوبِنَا بَضِيَاءَ
نَظَرِهَا إِلَيْكَ حَتَّى تَخْرِقَ أَبْصَارَ الْقُلُوبِ حُجُبَ النُّورِ فَتَصِلَ إِلَيَّ
مَعْدِنَ الْعِظْمَةِ وَتَصِيرَ أَرْوَاحَنَا مُعَلَّقَةً بِعِزِّ قُدْسِكَ

“Mola Wangu mimi ni mja Wako dhaifu mtenda dhambi, mtumwa Wako niliyerejea, basi usinijaalie kuwa ni yule uliyemgeuzia uso Wako, na ikamzuia sahu yake kutaka msamaha Wako. Mola Wangu nipe ukamilfu wa kufikia Kwako, yanawirishe maono ya nyoyo zetu kwa mwanga unaoangazia

Kwako, hadi kupenya mapazia ya nuru yafikie asili ya utukufu, na roho zetu ziwe zaning'inia kwa ezi ya utakatifu Wako.

إِلَهِي وَجَعَلَنِي مِمَّنْ نَادَيْتُهُ فَأَجَابَكَ وَلَا حَظَّتُهُ فَصَعِقَ لِجَلَالِكَ
فَنَاجَيْتُهُ سِرًّا وَعَمِلَ لَكَ جَهْرًا إِلَهِي لَمْ أُسَلِّطْ عَلَى حُسْنِ ظَنِّي
قُنُوطَ الْأَيَّاسِ وَلَا انْقَطَعَ رَجَائِي مِنْ جَمِيلِ كَرَمِكَ

“Mola wangu nijaalie kuwa ni Uliyemwita akakuitika, na Ukamtupia jicho akashangazwa kwa utukufu Wako, ukamnong'oneza kwa siri akakutekelezea kwa jahara. Mola Wangu sikuusaliti wema wa dhana yangu kwa kuvunjika moyo na kukata tamaa, na sikuacha kutarajia wema wa ukarimu Wako.

إِلَهِي إِنْ كَانَتْ الْخَطَايَا قَدْ أَسْقَطْتَنِي لَدَيْكَ فَاصْفَحْ عَنِّي
بِحُسْنِ تَوَكُّلٍ عَلَيْكَ إِلَهِي إِنْ حَطَّيْتَنِي الذُّنُوبُ مِنْ مَكَارِمِ
لُطْفِكَ فَقَدْ نَبَّهَنِي الْيَاقِينَ إِلَى كَرَمِ عَطْفِكَ إِلَهِي إِنْ أَنَامْتَنِي
الْعَفْلَةَ عَنِ الْإِسْتِعْدَادِ لِلِقَائِكَ فَقَدْ نَبَّهَنِي الْمَعْرِفَةَ بِكَرَمِ أَلْيَتِكَ
إِلَهِي إِنْ دَعَانِي إِلَى النَّارِ عَظِيمٍ عِقَابِكَ فَقَدْ دَعَانِي إِلَى الْجَنَّةِ
جَزِيلِ ثَوَابِكَ

“Mola wangu iwapo makosa yangu yamenidhili mbele Zako, basi niwelee radhi kwa wema wa utegemevu wangu Kwako. Mola Wangu iwapo dhambi zangu zimenitenga mbali na upole

wa huruma Yako, basi imenizindua yakini kwa upenu bora Wako. Mola Wangu iwapo imenilaza sahai yangu kutazamia kukutana Nawe, basi yamenizindua maarifa kwa utukufu wa neema Zako. Mola Wangu adhabu Yako kali inivutiapo motoni, basi wingi wa malipo Yako mema yamenivutia Peponi.

إِلٰهِي فَايَاكَ أَسْأَلُ وَإِلَيْكَ أَبْتَهِلُ وَأَرْغَبُ أَنْ تُصَلِّيَ عَلَيَّ مُحَمَّدٍ
وَأَلِ مُحَمَّدٍ وَأَنْ تَجْعَلَنِي مِمَّنْ يُدِيمُ ذِكْرَكَ وَلَا يَنْقُصُ عَهْدَكَ
وَلَا يَغْفُلُ عَنْ شُكْرِكَ وَلَا يَسْتَحْفِ بِأَمْرِكَ إِلٰهِي وَالْحَقْنِي بِنُورِ
عِزِّكَ الْأَبْهَجِ فَأَكُونَ لَكَ عَارِفًا وَعَنْ سِوَاكَ مُنْحَرِفًا وَمِنْكَ خَائِفًا
مُرَاقِبًا يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

“Mola Wangu nakuomba Wewe tu na kwa unyenyekevu nakutaka na napendekeza Umrehemu Muhammad na Aalize Muhammad, unijaalie niwe miongni mwa wenye kudumisha ukumbusho Wako, na hawatangui ahadi zao Kwako na hawa-sahau kukushukuru wala hawadharau amri Yako. Mola Wan-gu niambatisha kwa nuru ya enzi Yako inayong’ara nikujue Wewe nimkanushe asiyekuwa Wewe. Niwe ni mwenye kuji-hofia na kujichunga Kwako Ewe Mwenye ukuu na utukufu.

وَصَلَّى اللَّهُ عَلَيَّ مُحَمَّدٍ رَسُولِهِ وَإِلَيْهِ الطَّاهِرِينَ وَسَلِّمَ تَسْلِيمًا
كَثِيرًا.

“Mwenyezi Mungu amteremshie Mtume Wake Muham-mad na aali zake watakatifu rehema nyingi na amani kamili.”

SWALA YA MTUME (S.A.W.W.) KATIKA MWEZI WA SHAABANI

Hii ni swala ya kumtakia Bwana Mtume rehema katika mwezi wa Shaabani. Imepokewa kwamba Imam Zaynul Abidiin alikuwa akiisoma katika kipindi cha zawaal (jua kichwani) kila siku na pia akiisoma usiku wa Nisfus-Shabaan.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ شَجَرَةَ النَّبُوَّةِ وَمَوْضِعِ
الرِّسَالَةِ وَمُخْتَلَفِ الْمَلَائِكَةِ وَمَعْدِنِ الْعِلْمِ وَأَهْلِ بَيْتِ الْوَحْيِ

“Ewe Mwenyezi Mungu mrehemu Muhammad na Aalize Muhammad ukoo wa Utume, makao ya Ujumbe, makutano ya Malaika, na chimbuko la ilimu, na watu wa nyumba ya Wahyi.

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ الْفُلْكِ الْجَارِيَةِ فِي الْلُحْجِ
الْغَامِرَةِ يَأْمَنُ مَنْ رَكَبَهَا وَيَغْرُقُ مَنْ تَرَكَهَا، أَلْتَقَدَّمْ لَهُمْ مَارِقٌ
وَأَلْتَأَخَّرْ عَنْهُمْ زَاهِقٌ وَأَلْلَازِمٌ لَهُمْ لَاحِقٌ

“Ewe Mwenyezi Mungu mrehemu Muhammad na Aalize Muhammad, safina inayoelea juu ya mawimbi ya ba-

hari iliyotanda na kina kirefu, wakuokoka ni aliyeipanda na wakughariki ni anayeiyepuka, na mwenye kuwatangulia mbele atapotea na mwenye kusalia nyuma yao atangamia, na mwenye kuwa na wao ameunga.

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ الْكَهْفِ الْحَصِينِ، وَغِيَاثِ
الْمُضْطَرِّ الْمُسْتَكِينِ، وَمَلَجِ الْأَهَارِيِّينَ وَعِصْمَةِ الْمُعْتَصِمِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu mrehemu Muhammad na aalize Muhammad, ngome iliyo madhubuti, muokozi wa walio mashakani wanaobeheneka. Hamio la kuwasitiri wakimbizi na pa usalama kwa wenye kujihifadhi.

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ صَلَاةً كَثِيرَةً تَكُونُ لَهُمْ
رِضًا وَلِحَقِّ مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ أَدَاءً وَقَضَاءً بِحَوْلِ مِنْكَ وَقُوَّةِ
يَا رَبَّ الْعَالَمِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu mrehemu Muhammad na Aalize Muhammad, rehema nyingi mno zenye kuwaridhisha, na ni haki ya Muhammad na Aalize Muhammad kulipwa na kutimiziwa, kwa namna na uweza Wako, Ewe Bwana Mlezi wa viumbe vyote pia.

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ الطَّيِّبِينَ الْأَبْرَارِ الْأَخْيَارِ
الَّذِينَ أَوْجَبْتَ حُقُوقَهُمْ وَفَرَضْتَ طَاعَتَهُمْ وَوَلَّيْتَهُمْ

“Ewe Mwenyezi Mungu mrehemu Muhammad na Aalize Muhammad, wema watenda mema walio bora. Ambao ume-wajibisha haki zao, na ukafaradhisha kutwiiwa wao na ku-fuata uongozi wao.

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ وَأَعْمُرْ قَلْبِي بِطَاعَتِكَ
وَلَا تُخْزِنِي بِمَعْصِيَتِكَ وَأَرْزُقْنِي مُوَأَسَاةَ مَنْ قَتَرْتَ عَلَيْهِ مِنْ
رِزْقِكَ بِمَا وَسَعَتْ عَلَيَّ مِنْ فَضْلِكَ وَنَشَرْتَ عَلَيَّ مِنْ عَدْلِكَ
وَأَحْيَيْتَنِي تَحْتَ ظِلِّكَ

“Ewe Mwenyezi Mungu mrehemu Muhammad na Aalize Muhammad, uimarisha moyo wangu uwe mtwifu Kwako, wala usinihizi Kwako kwa kukuasi. Uniruzuku wasaa wa riziki iliyonifinyikia, kama ulivyonipanulia fadhila Zako na ukani-fungulia uadilifu Wako ukanipa maisha chini ya kivuli Chako.

وَهَذَا شَهْرُ نَبِيِّكَ سَيِّدِ رُسُلِكَ شَعْبَانَ الَّذِي حَفَفْتَهُ مِنْكَ
بِالرَّحْمَةِ وَالرِّضْوَانِ الَّذِي كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ
وَسَلَّمَ يَدْأَبُ فِي صِيَامِهِ وَقِيَامِهِ فِي لَيَالِيهِ وَأَيَّامِهِ نُجُوعًا لَكَ فِي

إِكْرَامِهِ وَإِعْظَامِهِ إِلَىٰ مَحَلِّ حَمَامِهِ

“Na huu ni mwezi wa Mtume Wako Bwana wa Mitume, Shaabani ambao umeutandazia rehema na maridhawa kutoka Kwako. Ambapo Mtume wa Mwenyezi Mungu rehema zimshukie yeye na Aalize, alijitahidi kuufunga kwa ajili Yako na kusimama (kwa ibada) katika nyusiku zake na michana yake. Alipenda kuweka athari nzuri akiutukuza na kuuadhimisha kwa ajili Yako mpaka kufikia kituo cha mauti yake.

اللَّهُمَّ فَأَعِنَّا عَلَىٰ الْإِسْتِنَانِ بِسُنَّتِهِ فِيهِ وَنَيْلِ الشَّفَاعَةِ لَدَيْهِ أَللَّهُمَّ
وَأَجْعَلْهُ لِي شَفِيعًا مُّشَفِّعًا وَطَرِيقًا إِلَيْكَ مَهِيْعًا وَأَجْعَلْنِي لَهُ مُتَّبِعًا
حَتَّىٰ أَلْقَاكَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَنِّي رَاضِيًا وَعَنْ ذُنُوبِي غَاضِيًا قَدْ
أَوْجَبْتَ لِي مِنْكَ الرَّحْمَةَ وَالرُّضْوَانَ وَأَنْزَلْتَنِي دَارَ الْقَرَارِ وَمَحَلَّ
الْأَخْيَارِ

“Ewe Mwenyezi Mungu basi tusaidie humo tuitekeleze Sunnah yake, na kunali shafaa kutoka kwake. Ewe Mwenyezi Mungu nijaaliye shufaa nafuu na njia ya kukufikia iwe ni mapitio maarufu na mapana. Na nijaalie nishikamane naye mpaka nikutane Nawe Siku ya Kiyama uwe umeridhika nami na madhambi yangu umeyasitiri. Umeniwajibishia rehema na radhi, na ukanipokea katika nyumba ya makao ya watu bora.”

DUA ZA MWEZI WA RAMADHANI

SOMA DUA HIZI BAADA YA KILA SWALA YA FARADHI KATIKA MWEZI WA RAMADHANI

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ
يَا عَلِيُّ يَا عَظِيمُ يَا غَفُورُ يَا رَحِيمُ أَنْتَ الرَّبُّ الْعَظِيمُ الَّذِي
لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Ewe Mtukufu, Ewe Mkuu, Ewe Msamehevu, Ewe Mrehe-
mevu. Ndiwe Bwana Mlezi Mkuu, Asiyefanana na chochote,
Yeye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona.

وَهَذَا شَهْرٌ عَظُمَتْهُ وَكَرَّمَتْهُ وَشَرَّفَتْهُ وَفَضَّلَتْهُ عَلَى الشُّهُورِ

“Na huu ni mwezi umeuadhimisha na umeutukuza,
umeuthaminisha na umeufadhilisha kuliko miezi yote.

وَهُوَ الشَّهْرُ الَّذِي فَرَضَتْ صِيَامَهُ عَلَيَّ وَهُوَ شَهْرُ رَمَضَانَ

Nao ni mwezi ambao umenifaridhia kufunga, nao ni mwe-
zi wa Ramadhani

الَّذِي أَنْزَلَتْ فِيهِ الْقُرْآنَ هُدًى لِلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَى
وَالْفُرْقَانِ

“Ambamo umeiteremsha humo Qur’ani yenye kuwaongoa watu na yenye kudhihirisha wazi uwongofu na upambanuzi.

وَجَعَلْتَ فِيهِ لَيْلَةَ الْقَدْرِ وَجَعَلْتَهَا خَيْرًا مِّنْ أَلْفِ شَهْرٍ

“Na umejaalia humo Usiku wa Cheo na umejaalia kuwa ni bora kuliko miezi elfu.

يَا ذَا الْأَمْنِ وَلَا يُمْنُ عَلَيْكَ مَنَّ عَلَيَّ بِفِكَائِكَ رَقَبَتِي مِنَ النَّارِ
فِيْمَنْ تَمُنُّ عَلَيْهِ

“Basi Ewe Mwenye kuneemesha usiyeneemeshwa, nineemeshe kwa kuniachilia huru mbali na Moto nikiwa pamoja na unaowaneemesha.

وَأَدْخِلْنِي الْجَنَّةَ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ.

“Na uniingize Peponi kwa rehema Zako Ee Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.”

**PIA SOMA DUA HII KILA BAADA YA
SWALA ZA FARADHI KATIKA MWEZI WA
RAMADHANI.**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

اللَّهُمَّ أَدْخِلْ عَلَيَّ أَهْلَ الْقُبُورِ السُّرُورَ

Ewe Mwenyezi Mungu waingizie furaha waliomo makuburini,

اللَّهُمَّ أَغْنِ كُلَّ فَقِيرٍ

Ewe Mwenyezi Mungu Mtajirisha kila fakiri,

اللَّهُمَّ أَشْبِعْ كُلَّ جَائِعٍ

Ewe Mwenyezi Mungu mshibisha kila mwenye njaa,

اللَّهُمَّ اكْسُ كُلَّ عُرْيَانٍ

Ewe Mwenyezi Mungu mvishe kila aliyeuchi,

اللَّهُمَّ اقْضِ دَيْنَ كُلِّ مَدِينٍ

Ewe Mwenyezi Mungu Mkidhie deni kila mdaiwa,

اللَّهُمَّ فَرِّجْ عَنَّا كُلَّ مَكْرُوبٍ

Ewe Mwenyezi Mungu Mfariji kila mwenye dhiki,

اللَّهُمَّ رُدِّ كُلَّ غَرِيبٍ

Ewe Mwenyezi Mungu mrejeshe kila aliye ugenini,

اللَّهُمَّ فَكِّ كُلَّ أَسِيرٍ

Ewe Mwenyezi Mungu mfungue kila mfugwa

اللَّهُمَّ أَصْلِحْ كُلَّ فَاسِدٍ مِنْ أُمُورِ الْمُسْلِمِينَ

Ewe Mwenyezi Mungu yatengeneze kila yaliyoharibika katika mambo ya Waislamu,

اللَّهُمَّ اشْفِ كُلَّ مَرِيضٍ

Ewe Mwenyezi Mungu mponye kila mgonjwa

اللَّهُمَّ سُدِّ فَقْرَنَا بِغِنَاكَ

Ewe Mwenyezi Mungu tuzibie ufakiri wetu kwa utajiri Wako,

اللَّهُمَّ غَيِّرْ سُوءَ حَالِنَا بِحُسْنِ حَالِكَ

Ewe Mwenyezi Mungu ubadilishe uovu wa hali zetu kwa wema wa hali Yako,

اللَّهُمَّ أَقْضِ عَنَّا الدَّيْنَ وَأَغْنِنَا مِنَ الْفَقْرِ إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

Ewe Mwenyezi Mungu tukidhie deni zetu, Na ututajirishe tutoke kwenye umasikini, Hakika wewe Unauweza juu ya kila kitu

DUA ZA SIKU MAALUMU ZA MWEZI MTUKUFU WA RAMADHANI ALIZOKUWA AKIZISOMA BWANA MTUME (S.A.W.W.)

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

DUA YA SIKU YA 1

اَللّٰهُمَّ اَجْعَلْ صِيَامِي فِيهِ صِيَامَ الصَّائِمِيْنَ وَقِيَامِي فِيهِ قِيَامَ
الْقَائِمِيْنَ وَتَبِّهْنِي فِيهِ عَنِ نَوْمَةِ الْغَافِلِيْنَ وَهَبْ لِي جُرْمِي فِيهِ يَا
اِيْلَهَ الْعَلَمِيْنَ وَاَعْفُ عَنِّي يَا عَافِيًّا عَنِ الْمُجْرِمِيْنَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, ijaalie katika siku hii fungu yangu ni saumu ya wafungao, kusimama kwangu kuwe ni msimamo vilivyo wafanyi ibada, na Nitanabahisha na usingizi wa wavivu. Nisamehe makosa yangu, Ewe Mola wa walimwengu na uniafu, Ewe Mwenye kuwaafu wakosaji.”

DUA YA SIKU YA 2

اَللّٰهُمَّ قَرِّبْنِي فِيهِ اِلَى مَرْضَاتِكَ وَجَنِّبْنِي فِيهِ مِنْ سَخَطِكَ
وَنِقْمَاتِكَ وَوَفِّقْنِي فِيهِ لِقِرَاءَةِ آيَاتِكَ بِرَحْمَتِكَ يَا اَرْحَمَ الرَّاحِمِيْنَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, Nikurubishe katika siku hii kwenye radhi Zako, niepushie hasira Zako na ghadhabu Zako na uniwafikie nizisome Aya Zako, kwa rehema Zako, Ewe Mwingi wa kurehemu.”

DUA YA SIKU YA 3

اللَّهُمَّ ارْزُقْنِي فِيهِ الذُّهْنَ وَالتَّنْبِيَهَ وَبَاعِدْنِي فِيهِ مِنَ السَّفَاهَةِ
وَالتَّمَوِيهِ وَاجْعَلْ لِي نَصِيبًا مِنْ كُلِّ خَيْرٍ تُنْزِلُ فِيهِ بِجُودِكَ يَا
أَجُودَ الْأَجُودِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, niruzuku katika siku hii uekevu na uzinduko, niepushie mbali ubaradhuli na upumbavu, na unijaalie kupata fungu la kila kheri inayoteremka humo kwa ukarimu Wako, Ewe Mwingi wa ukarimu.”

DUA YA SIKU YA 4

اللَّهُمَّ قَوِّنِي فِيهِ عَلَى إِقَامَةِ أَمْرِكَ وَأَذِقْنِي فِيهِ حَلَاوَةَ ذِكْرِكَ
وَأَوْزِعْنِي فِيهِ لِأَدَاءِ شُكْرِكَ بِكَرَمِكَ وَأَحْفَظْنِي فِيهِ بِحِفْظِكَ
وَسِتْرِكَ يَا أَبْصَرَ النَّاطِرِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, niwezesha katika siku hii kushika amri Zako, unionjeshe utamu wa utajo Wako, na uniwezeshe kutekeleza wajibu wa kukushukuru kwa ukarimu Wako. Ni-

hifadhi kwa ulinzi Wako na sitara Yako, Ewe Muona zaidi ya wanaoangalia.”

DUA YA SIKU YA 5

اللَّهُمَّ اجْعَلْنِي فِيهِ مِنَ الْمُسْتَغْفِرِينَ وَاجْعَلْنِي فِيهِ مِنْ عِبَادِكَ
الصَّالِحِينَ الْقَانِتِينَ وَاجْعَلْنِي فِيهِ مِنْ أَوْلِيَائِكَ الْمُقَرَّبِينَ بِرَأْفَتِكَ
يَا أَرْحَمَ الرَّحِمِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, nijaalie katika siku hii niwe miongoni mwa wanaoomba maghufira na uniweke miongoni mwa waja Wako wema walio wanyenyekvu. Na unijaalie niwe miongoni mwa mawalii Wako karibu Nawe, kwa huruma Yako Ewe Mwingi wa kurehemu.”

DUA YA SIKU YA 6

اللَّهُمَّ لَا تَخْذُلْنِي فِيهِ لِتَعَرُّضِ مَعْصِيَتِكَ وَلَا تَضْرِبْنِي بِسَيِّئِ
نَقْمَتِكَ وَزَحْزِحْنِي فِيهِ مِنْ مُوجِبَاتِ سَخَطِكَ بِمَنِّكَ وَأَيَادِيكَ
يَا مُنْتَهَى رَغْبَةِ الرَّاعِبِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, usinidhalilishe katika siku hii hata nimili kukuasi, na wala usinichape kwa mbati za adhabu Yako, uniepushie mbali yanayonitakia hasira Zako; kwa neema Zako na vipawa Vyako Ewe Mkusudiwa maombi ya waombaji.”

DUA YA SIKU YA 7

اللَّهُمَّ أَعِنِّي فِيهِ عَلَى صِيَامِهِ وَقِيَامِهِ وَجَنِّبِي فِيهِ مِنْ هَفَوَاتِهِ
وَأَثَامِهِ وَأَرْزُقْنِي فِيهِ ذِكْرَكَ بِدَوَامِهِ بِتَوْفِيقِكَ يَا هَادِيَ الْمُضِلِّينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, Nipe katika siku hii nguvu za kufunga na kuisimama kwa ibada na uniepushe na makosa na madhambi, unirusuku ukumbusho Wako daima kwa taufiki Yako, Ewe mwenye kuwaongoa wapotevu.”

DUA YA SIKU YA 8

اللَّهُمَّ أَرْزُقْنِي فِيهِ رَحْمَةَ الْإِيْتَامِ وَإِطْعَامَ الطَّعَامِ وَإِفْشَاءَ السَّلَامِ
وَصُحْبَةَ الْكِرَامِ بِطَوْلِكَ يَا مَلْجَأَ الْأَمِلِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, Niwezeshe katika siku hii niwarehemu mayatima na nilishe vyakula, Nitoe salamu na nisuhubiane na watu wema kwa ukunjufu Wako, Ewe Makimbilio ya wahitaji.”

DUA YA SIKU YA 9

اللَّهُمَّ اجْعَلْ لِي فِيهِ نَصِيبًا مِنْ رَحْمَتِكَ الْوَاسِعَةِ وَأَهْدِنِي فِيهِ
 لِبَرَاهِينِكَ السَّاطِعَةِ وَخُذْ بِنَاصِيَتِي إِلَى مَرْضَاتِكَ الْجَامِعَةِ
 بِمَحَبَّتِكَ يَا أَمَلَ الْمُشْتَاقِينَ

Ewe Mwenyezi Mungu, Nijaalie katika siku hii fungu la re-hema Zako enevu, uniongoze kwa buruhani Yako inayong'ara na uniendeshe kwenye mkusanyo wa maridhia Yako, kwa mahaba Yako, Ewe Tumaini la wenye shauku.”

DUA YA SIKU YA 10

اللَّهُمَّ اجْعَلْنِي فِيهِ مِنَ الْمُتَوَكِّلِينَ عَلَيْكَ وَاجْعَلْنِي فِيهِ مِنْ
 الْفَائِزِينَ لَدَيْكَ وَاجْعَلْنِي فِيهِ مِنَ الْمُقْرَبِينَ إِلَيْكَ بِإِحْسَانِكَ يَا
 غَايَةَ الطَّالِبِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, nijaalie katika siku hii niwe ni mwenye kukutegemea, Unijaalie ni mwenye kufuzu Kwako na Unijaalie niwe miongoni mwa wanao kurubishwa Kwako, kwa Yako hisani, Ee Kusudio la wahitaji.”

DUA YA SIKU YA 11

اللَّهُمَّ حَبِّ إِلَيَّ فِيهِ الْإِحْسَانَ وَكَرَهُ إِلَيَّ فِيهِ الْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ
وَحَرَّمَ عَلَيَّ فِيهِ السَّخَطَ وَالنِّيْرَانَ بِعَوْنِكَ يَا غِيَاثَ الْمُسْتَغِيثِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, nipendekeshe katika siku hii kutenda mema na unifanye nichukie upotovu na uasi, Nikinge na hasira Zako na Moto kwa muawana Wako Ewe Msaidizi wa waombao usaidizi.”

DUA YA SIKU YA 12

اللَّهُمَّ زَيِّنِي فِيهِ بِالسَّتْرِ وَالْعَفَافِ وَأَسْتُرْنِي فِيهِ بِلِبَاسِ الْقُنُوعِ
وَالْكَفَافِ وَأَحْمِلْنِي فِيهِ عَلَى الْعَدْلِ وَالْإِنصَافِ وَأَمِّنِّي فِيهِ مِنْ
كُلِّ مَا أَخَافُ بِعِصْمَتِكَ يَا عِصْمَةَ الْخَائِفِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, nipambe katika siku hii kwa sitara na utakatifu, na unisitiri kwa vazi la ukinaifu na kutosheka, na unisimamishe juu ya uadilifu na usawa, unisalimishe na kila niogopalo kwa hifadhi Yako, Ewe Mhifadhi wa wenye kuogopa.”

DUA YA SIKU YA 13

اللَّهُمَّ طَهِّرْنِي فِيهِ مِنَ الدَّنَسِ وَالْأَقْدَارِ وَصَبِّرْنِي فِيهِ عَلَى كَائِنَاتِ
الْأَقْدَارِ وَوَفِّقْنِي فِيهِ لِلتَّقَى وَصُحْبَةِ الْأَبْرَارِ بِعَوْنِكَ يَا قُرَّةَ عَيْنِ
الْمَسَاكِينِ

“Ewe Mwenyezi Mungu, nitakase katika siku hii na uchafu na taka, unipe subira juu ya matukio na kadura, na uniwafikie hadhari na nisuhubiane na watu wema kwa usaidizi Wako, Ewe Mburudisha macho ya masikini.”

DUA YA SIKU YA 14

اللَّهُمَّ لَا تُؤْخِذْنِي فِيهِ بِالْعَثَرَاتِ وَأَقْلِنِي فِيهِ مِنَ الْخَطَايَا
وَالْهَفْوَاتِ وَلَا تَجْعَلْنِي فِيهِ غَرَضًا لِلْبَلَايَا وَالْآفَاتِ بِعِزَّتِكَ يَا عِزَّ
الْمُسْلِمِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, Usinipatilize katika siku hii niki-sepetuka, na Nififishie makosa na telezi, na Usinijaalie kuwa na shabaha ya kuzuwa balaa na maafa, kwa Ezi Yako, Ewe Utukufu wa Waislamu.

DUA YA SIKU YA 15

اللَّهُمَّ ارْزُقْنِي فِيهِ طَاعَةَ الْخَاشِعِينَ وَأَشْرَحْ فِيهِ صَدْرِي بِإِنَابَةٍ
الْمُخْتَبِينَ بِأَمَانِكَ يَا أَمَانَ الْخَائِفِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, Niruzuku katika siku hii utwiifu wa wanaochelea, na unipanue kifua changu kwa majuto ya wanyenyekevu, kwa amani Yako, Ewe Amani kwa wenye kuogopa.

DUA YA SIKU YA 16

اللَّهُمَّ وَفَّقْنِي فِيهِ لِمُؤَافَقَةِ الْأَبْرَارِ وَجَنِّبْنِي فِيهِ مُرَافَقَةَ الْأَشْرَارِ
وَأُونِي فِيهِ بِرَحْمَتِكَ إِلَى دَارِ الْقَرَارِ بِالْهَيْتِكَ يَا إِلَهَ الْعَالَمِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, niwafkie katika siku hii niwe sawa na watu wema na unitenge na kuwarafiki waovu, Unipokee kwa rehema Zako katika nyumba ya utulivu kwa Uungu Wako, Ewe Mwenyezi Mungu wa viumbe vyote.”

DUA YA SIKU YA 17

اللَّهُمَّ اهْدِنِي فِيهِ لِصَالِحِ الْأَعْمَالِ وَأَقْضِ لِي فِيهِ الْحَوَائِجَ
وَالْأَمَالَ يَا مَنْ لَا يَحْتَاجُ إِلَى التَّفْسِيرِ وَالسُّؤَالِ يَا عَالِمًا بِمَا فِي
صُدُورِ الْعَلَمِينَ صَلَّى عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ الطَّاهِرِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, niongoze katika siku hii kwa ama-
li njema na nitimize haja zangu na matumaini yangu, Ewe
usiyehitajia maelezo na hoja. Ewe Mjuzi wa yaliyomo katika
vifua vya walimwengu, Mteremshie rehema Muhammad na
Aali zake watakatifu.”

DUA YA SIKU YA 18

اللَّهُمَّ نَبِّهْنِي فِيهِ لِبَرَكَاتِ أَسْحَارِهِ وَنُورِ قَلْبِي فِيهِ بِضِيَاءِ أَنْوَارِهِ
وَخُذْ بِكُلِّ أَعْضَائِي إِلَى التَّبَاعِ آثَارِهِ بِنُورِكَ يَا مُنُورَ قُلُوبِ
الْعَارِفِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, nitanabahishe katika siku hii
nipate baraka za nyusiku zake na unawirishe moyo wangu
humo kwa mwangaza wa nuru yake. Na Vipatilize viungo vy-
angu vifuate athari zake, kwa nuru Yako, Ewe Mnawirisha
nyoyo za wajuzi.

DUA YA SIKU YA 19

اللَّهُمَّ وَفِّرْ فِيهِ حَظِّي مِنْ بَرَكَاتِهِ وَسَهِّلْ سَبِيلِي إِلَىٰ خَيْرَاتِهِ وَلَا
تَحْرِمْنِي قَبُولَ حَسَنَاتِهِ يَا هَادِيًا إِلَىٰ الْحَقِّ الْمُبِينِ

“Ewe Mwenyezi Mungu, likuze katika siku hii fungu langu la baraka zake na unisahilishie njia ya kuyafikia mema yake na usininyime kabuli ya njema zake, Ewe Muongoaji kwenye haki iliyobayana.

DUA YA SIKU YA 20

اللَّهُمَّ افْتَحْ لِي فِيهِ أَبْوَابَ الْجَنَانِ وَأَغْلِقْ عَنِّي فِيهِ أَبْوَابَ النَّيرانِ
وَوَفِّقْنِي فِيهِ لِتِلَاوَةِ الْقُرْآنِ يَا مُنْزِلَةَ السَّكِينَةِ فِي قُلُوبِ الْمُؤْمِنِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, nifungulie katika siku hii milango ya Peponi na unifungie milango ya Motoni na niwafikie kusoma Qur’ani, Ewe Mteremsha utulivu nyoyoni mwa Waumini.

DUA YA SIKU YA 21

اللَّهُمَّ اجْعَلْ لِي فِيهِ إِلَى مَرْضَاتِكَ دَلِيلًا وَلَا تَجْعَلْ لِلشَّيْطَانِ فِيهِ
عَلَى سَبِيلًا وَاجْعَلْ الْجَنَّةَ لِي مَنزِلًا وَمَقِيلًا يَا قَاضِيَ حَوَائِجِ
الطَّالِبِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, nionyesha katika siku hii njia ya kupata radhi Zako na usimpe Shetwani uweza juu yangu, uijaalie Pepo ni mashukio na mapumziko yangu, Ewe Mtekeleza haja za waombaji.”

DUA YA SIKU YA 22

اللَّهُمَّ افْتَحْ لِي فِيهِ أَبْوَابَ فَضْلِكَ وَأَنْزِلْ عَلَيَّ فِيهِ بَرَكَاتِكَ
وَوَفِّقْنِي فِيهِ لِمُوجِبَاتِ مَرْضَاتِكَ وَأَسْكِنِّي فِيهِ بُحْبُوحَاتِ جَنَّتِكَ
يَا مُجِيبَ دَعْوَةِ الْمُضْطَرِّينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, nifungulie katika siku hii milango ya fadhila Zako na uniteremshie baraka Zako, Niwafikie yanayonileta kwenye radhi Zako na unituze katika ustawi wa Pepo Yako Ewe Mwitikia maombi ya walio mashakani.”

DUA YA SIKU YA 23

اللَّهُمَّ اغْسِلْنِي فِيهِ مِنَ الذُّنُوبِ وَطَهِّرْنِي فِيهِ مِنَ الْعُيُوبِ
وَأَمْتَحِنْ قَلْبِي فِيهِ بِتَقْوَى الْقُلُوبِ يَا مُقِيلَ عَثَرَاتِ الْمُذْنِبِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, nitakase katika siku hii nitoke dhambini, unitakase mbali na aibu na ukague moyo wangu humo kwa nyoyo za takwa, Ewe Mwenye kuyapuuza madhambi ya wenye kuteleza.”

DUA YA SIKU YA 24

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ فِيهِ مَا يُرْضِيكَ وَأَعُوذُ بِكَ مِمَّا يُؤْذِيكَ
وَأَسْأَلُكَ التَّوْفِيقَ فِيهِ لِأَنْ أُطِيعَكَ وَلَا أَعْصِيكَ يَا جَوَادَ السَّائِلِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, nakuomba katika siku hii yanayokuridhisha na najilinda Kwako na yanayokuudhi, nakuomba uniwafikie nikutii nisikuasi; Ewe Mpaji wa wanaoomba.”

DUA YA SIKU YA 25

اللَّهُمَّ اجْعَلْنِي فِيهِ مُحِبًّا لِأَوْلِيَائِكَ وَمُعَادِيًّا لِأَعْدَائِكَ مُسْتَنًا بِسُنَّةِ
خَاتَمِ أَنْبِيَائِكَ يَا عَاصِمَ قُلُوبِ النَّبِيِّينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, nijaalie katika siku hii niwe ni mwenye kuwapenda mawalii Wako, na niwachukie maadui Zako, nikifuata mwendo wa Mtume Wako wa mwisho, Ewe Muhifadhi nyoyo za Mitume.”

DUA YA SIKU YA 26

اللَّهُمَّ اجْعَلْ سَعْيِي فِيهِ مَشْكُورًا وَذَنْبِي فِيهِ مَغْفُورًا وَعَمَلِي فِيهِ
مَقْبُولًا وَعَيْبِي فِيهِ مَسْتُورًا يَا أَسْمَعَ السَّمْعِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, Ijaalie katika siku hii hima yangu ni ya kuthaminiwa, na dhambi zangu ni za kusamehewa, na amali zangu ni za kukubaliwa na aibu zangu ni za kusitiriwa; Ewe Msikizi zaidi ya wanaosikiza.”

DUA YA SIKU YA 27

اللَّهُمَّ ارْزُقْنِي فِيهِ فَضْلَ لَيْلَةِ الْقَدْرِ وَصَيْرْ أُمُورِي فِيهِ مِنَ الْعُسْرِ
إِلَى الْيُسْرِ وَأَقْبَلْ مَعَاذِيرِي وَحُطِّ عَنِّي الذَّنْبَ وَالْوِزْرَ يَا رَوْفًا
بِعِبَادِهِ الصَّالِحِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, niruzuku katika siku hii fadhila za Laylatul Qadri na nipindulie mambo yangu mazito yawe

mepesi, Nikubalie nyudhuru zangu na nifutie madhambi na makosa, Ewe Mpole kwa waja Wake wema.”

DUA YA SIKU YA 28

اللَّهُمَّ وَفِّرْ حَظِّي فِيهِ مِنَ النِّوَافِلِ وَأَكْرِمْنِي فِيهِ بِإِحْضَارِ الْمَسَائِلِ
وَقَرِّبْ فِيهِ وَسِيلَةَ إِلَيْكَ مِنْ بَيْنِ الْوَسَائِلِ يَا مَنْ لَا يَشْعَلُهُ الْإِحَاحُ
الْمُلْحِينِ

“Ewe Mwenyezi Mungu, lizidishe katika siku hii fungu langu kwa naafila na unikirimu, niyashughulikie majukumu yangu na unifanyie karibu njia ya kukufikia kwa njia mbalimbali, Ewe Usiyeshughulishwa na himiza za wenye kuhimiza.”

DUA YA SIKU YA 29

اللَّهُمَّ غَشِّنِي فِيهِ بِالرَّحْمَةِ وَأَرْزُقْنِي فِيهِ التَّوْفِيقَ وَالْعِصْمَةَ وَطَهِّرْ
قَلْبِي مِنْ غِيَاهِبِ التُّهْمَةِ يَا رَحِيمًا بَعْبَادِهِ الْمُؤْمِنِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, nitande katika siku hii kwa rehma, na uniruzuku tawfiki na hifadhi, na utakase moyo wangu kutokamana na giza la shaka, Ewe Mrehemevu wa waja Wako Waumini.”

DUA YA SIKU YA 30

اللَّهُمَّ اجْعَلْ صِيَامِي فِيهِ بِالشُّكْرِ وَالْقَبُولِ عَلَيَّ مَا تَرْضَاهُ
وَيَرْضَاهُ الرَّسُولُ مُحْكَمَةً فُرُوعِهِ بِالأُصُولِ بِحَقِّ سَيِّدِنَا مُحَمَّدًا
وآلِهِ الطَّاهِرِينَ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

Ee Mwenyezi Mungu, Ijaalie katika siku hii saumu yangu ni yenye kutambuliwa na kukubaliwa kwa namna unayoridhia na inayomridhisha Mtume, iwe na matawi thabiti kwa mashina kwa haki ya Bwana wetu Muhammad na kizazi chake kitakatifu.

Walhamdu Lillahi Rabbil Aalamiina.

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHJI

AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl

57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume – Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume – Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume – Umaasumu wa Mitume
Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah – Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah – Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Eflu – Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Eflu – Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Eflu – Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Eflu – Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Eflu – Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Eflu – Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio
njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-Ilaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi

86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqaalain
115. Maarifa ya Kiislamu

116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
(Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
(Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya — Wanawake katika Uislamu

145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt
(Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt
(Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an — Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka katika Qur'an — Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu — Sehemu ya
kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu — Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu — Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu — Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Mshumaa.
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi

173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na
Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Jihadi ya Imam Hussein ('as)
185. Kazi na kujituma ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib — Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Weledi juu ya Mustakabali
189. Usalafi — Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia — Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)

KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi